# RASIMU YA KATIBA YA TANZANIA SHARING ASSOCIATION

**Dira ya chama chetu:**

1. Kusaidiana katika shida na raha (Social Issues).
2. Kufanya mambo ya maendeleo na ustawi wa wanachama (Development Issues).
3. Kusaidia kutatua matatizo madogo madogo yatakayohitaji msaada katika jamii.

# APRIL 2019

# IBARA YA KWANZA

## 1. UTANGULIZI

Tanzania Sharing Association ni chama cha watanzania wenye **ASILI au NASABA** ya utanzania kwa kuzaliwa, kuoa au kuolewa, na jambo lingine lolote linaloweza kumpa haki ya uraia (kisheria) mtu anayejitambulisha kama mtanzania kwa kukili na kujitambua kuwa ni mtanzania, kuadaptiwa au kuzaliwa na mtanzania. Chama hiki kilianzishwa jijini Houston katika Jimbo la Texas tarehe **4/1/2019**. Baada ya mwaka mmoja, wanachama walikubaliana kukubali ndugu, jamaa na marafiki waishio majimbo tofauti ndani ya USA.

# IBARA YA PILI

## 2. JINA NA CHAMA

Jina la chama hiki litafahamika kama **Tanzania Sharing Association,** na kifupisho chake kitajulikana kama **TSA**.

# IBARA YA TATU

## 3. USAJILI, ANUANI, NA NEMBO YA CHAMA

### 3.1 Usajili

Chama hiki kimesajiliwa kama shirika lisilo na faida (Non profit Organization), vilevile kitakuwa ni chama huru kisicho cha serikali na kisichofungamana na chama chochote cha siasa, jamii, kabila na wala misingi ya dini yoyote. Chama kitaendesha shughuli zake kwa mujibu wa katiba na sheria za Texas.

### 3.2 Anuani

Ofisi ya chama itakuwa Houston Texas na itatumia anuani ya posta

PO BOX 720801<br>
Houston, TX 77072<br>
No. ya simu: 281-372-9205

Anuani hii itatumika mpaka hapo chama kitapofungua ofisi.

3.3 **Nembo ya Chama**

## IBARA YA NNE

**4. NIA NA MADHUMUNI YA CHAMA**

4.1 Kujenga moyo wa upendo na ushirikiano kwa taratibu, kanuni na sheria zilizowekwa baina na wanachama.

4.2 Kutiana moyo katika masuala yote yahusuyo elimu, biashara, kazi, taaluma na ustawi wa jamii kwa ujumla.

4.3 Kwa kuzingatia ibara ya 4.1, wanachama watapaswa kuzingatia yafuatayo:

Kusaidiana wakati wa shida. Hii itajumuisha masuala yote ambayo yanaweza kumfika mwanachama au ndugu waliokuwa kwenye mkataba kama **msiba, ugonjw**a (kuuguliwa na kukaa hospitali/Rehab, Therapy zaidi ya majuma 2), **kushikiliwa na uhamiaji, kuunguliwa na moto**.

- Katibu/Mhakiki ataomba nakala kama cheti cha kuzaliwa, nakala kutoka kwa daktari, nakala kutoka shule, nakala kutoka police, nakala kutoka uhamiaji, nakala kutoka kituo cha zima moto, nakala kutoka chumba cha kuhifadhia maiti n.k ili kuridhia nakutangaza shida hizo.
- Mwanachama atatakiwa kutoa taarifa za shida/msiba ndani ya siku 7.
- Mwanachama atasaidiwa kuandaa sherehe/maombi kwa kiasi cha **($300)** kama kutakuwa na sherehe/maombi kwa ajili ya shida/msiba.
    - Mwanachama anatakiwa kutoa taarifa siku 7 kabla ya sherehe hiyo na ndani ya siku 40 toka shida/msiba kutangazwa.
    - Mwanachama hatakabidhiwa pesa bali kiongozi husika atashirkiana na mwanachama kusimamia shughuli hiyo.

4.4 Kwa kuzingatia ibara ya 4.3, ndugu wanaokubalika ni kama wafuatayo:

- Wazazi/walezi wawili – Wazazi wa mwanachama au walezi wa mwanachama kama shangazi/mjomba/bibi/babu/binamu/wakwe n.k.
- Mume/mke mmoja – Mume/mke unaeishi naye, baba/mama watoto, rafiki unaeishi naye (boyfriend/girlfriend).
- Watoto – Wakuzaa mwenyewe, wa mume/mke, wa kaka/dada/mtoto aliefariki.
- Kaka/dada – Wa tumbo moja au wa baba (wakufikia).

4.5 Kwa kuzingatia ibara ya 4.3, jumla ya shida/msiba ni **5** ndani ya miaka **5** (**2020-2025**)

- 2 Shida ikiwemo msiba ndani ya mwaka na ikitokea zaidi itatangazwa **KIHIARI.**

**Uangalizi:** Hakutakuwa na ubadilishaji wa ndugu au kuongezwa isipokuwa watoto/dada/kaka watakaozaliwa, watoto wa kaka/dada au mtoto aliefariki. Mume/mke na watoto wao wanaweza badilishwa iwapo mume/mke hawajachangiwa. Na ikitokea wana watoto sio wakuwazaa, watoto wa mume/mke anayebadilishwa watatakiwa kuondolewa kwenye mkataba.

## IBARA YA TANO

### 5. UANACHAMA

5.1 **Chama hiki kitajumuisha wanachama wafuatao:**

- Wanachama waanzilishi.
- Wanachama waanzilishi waliohama USA.
- Wanachama wapya watakaojadiliwa na kukubaliwa na wanachama kwa asilimia isiyopungua 75 ndani ya siku 3.
- Wanachama wenye kupatwa na maradhi ya muda mrefu na kushindwa kushiriki kwa kutoa michango (Miezi 6).

5.2 **Sifa za Uanachama**

- Awe na akili timamu.
- Awe na umri usiopungua miaka 21.
- Akubaliane na kanuni na masharti mbali mbali kama yalivyoainishwa na katiba, sheria na nyaraka nyingine za chama.
- Awe na mahusiano mazuri pamoja na viongozi/wanachama wenzake.

### 5.3 Namna ya kujiunga na Chama

- Mwanachama atatakiwa kutoa kiingilio cha **$100**, akiba tangulizi ya kiasi cha **$100**, na kiasi cha **$25** kila mwaka.
  - Kiingilio cha **$100** na kiasi cha **$25** kila mwaka hazirejeshwi kwa mwanachama (Non refundable).
- Mwanachama atatakiwa kumaliza kulipa pesa zote ndani ya miezi 2 baada ya kukubalika.
- Chama kitaendelea kupokea wanachama wapya mara moja kwa mwezi.
- Uanachama utaanza rasmi baada ya miezi miwili na pale mwanachama atakapotia saini kwenye nakala zote na kukabidhi kwa kiongozi husika.
  - Kila mwanachama atatakiwa kutia saini nakala yeyote iwapo itahitajika.

### 5.4 Ukomo wa Uanachama

- Mwanachama kufariki.
- Kujihudhuru mwenyewe kwa hiari.
  - Atatakiwa kurudisha pesa yote aliochangiwa kutoa pesa aliochanga.
  - Atarudishiwa akiba yake tangulizi (advance).
  - Hatoruhusiwa kurudi kwenye chama mpaka muda wa **mwaka mmoja** na kuanza kama mwanachama mpya.
- Kufukuzwa uanachama iwapo ataonekana kupoteza sifa za uanachama.
  - Atatakiwa kurudisha pesa yote aliochangiwa kutoa pesa aliochanga.
  - Atarudishiwa akiba yake tangulizi. (Advance).
  - Hatoruhusiwa kurudi kwenye chama mpaka muda wa **mwaka mmoja** na kuanza kama mwanachama mpya.

### 5.5 Sababu za kusimamishwa uanachama na adhabu zake

5.5.1 Mwanachama atasimamishwa iwapo atafanya yafuatayo:

- Kutoheshimu uongozi na wanachama wote.
- Kutuma matangazo siku sizizo za matangazo zaidi ya mara 3.
- Kuleta mambo binafsi kwenye chama.
- Kutumia lugha isiyo sahihi na kuanzisha malumbano yasiohusiana na chama.
- Kushabikia mambo binafsi na kuendeleza malumbano zaidi ya mara 3.
- Kutawanya habari/sauti (siri) zinazohusiana na chama nnje ya chama.
- Mwanachama akihukumiwa na vyombo vya sheria kwa makosa yanayotishia amani ya wanachama (kama unyanyasaji wa kijinsia, unyanyasaji wa nyumbani, biashara ya ngono, ulevi, kushughulika na madawa ya kulevya, kuua kwa kusudia).
- Kujitoa (Exit) kwenye chama wakati wa mkutano.
  - Atakuwa na mkutano na Bodi ya Wadhamini na kupewa maamuzi.

5.5.2 Mwanachama atapewa warning zifuatazo:

- Kutaarifiwa kama amekosea na Afisa Uhusiano.
- Kuandikiwa barua na Makamu wa Mwenyekiti.
- Kuwa na mkutano na Bodi ya Utendaji.
    - Kutolewa kwenye chama kwa muda wa siku 30.
    - Kupewa taarifa zote kuhusiana na michango na kuchanga kama kawaida.
    - Kuruhusiwa kutoa taarifa za Shida/Msiba na kuchangiwa kama kawaida.

**Uangalizi:** Mwanachama huyu akirudia makosa na kusimamishwa zaidi ya mara 2, atatolewa kwenye chama na kutoruhusiwa kurudi kwenye chama.

# IBARA YA SITA

## 6 HAKI NA WAJIBU WA WANACHAMA

### 6.1 Kila mwanachama anayo haki ya:

- Kuwepo katika orodha ya wanachama.
- Kuangalia rekodi zote za chama kama vile taarifa za vikao vilivyopita, mikataba n.k.
- Kuhoji kuhusu mapato na matumizi ya chama.
- Kugombea nafasi za uongozi.
- Kunufaika na chama kwa mujibu wa katiba, kanuni na sheria.
- Haki sawa ya kuchangia mawazo ya uendeshaji wa chama kwa mujibu wa katiba, kanuni na sheria.
- Kutoa malalamiko ili yajadiliwe kwa uwazi na kupewa ufumbuzi ndani ya chama.
- Kupiga kura iwapo kura zitahitajika.

### 6.2 Kila mwanachama anatakiwa awajibike kama ifutavyo:

- Kuzifahamu, kutii na kuzifuata kanuni na sheria za chama.
- Kutumia lugha sahihi na kutoanzisha malumbano yasiohusiana na chama.
- Kulinda na kutunza heshima na amani ya chama kwa viongozi na wanachama.
- Kutunza na kutotawanya habari/sauti (siri) zinazohusiana na chama.
- Kutoa michango na ada kulingana na mahitaji na mienendo ya chama.
- Kujitoa kwa hali na mali, pamoja na muda wake katika kuhakikisha malengo ya chama yanaafikiwa.
- Kuhudhuria na kushiriki kikamilifu vikao vyote vitakavyo itishwa na chama (Vikao vinaweza kuwa vya online/whatsapp, simu au kukutana).

- Kuchangia ufahamu na uzoefu kwa faida ya chama, wanachama wake na jamii inayozunguka chama hiki.
- Kutoa taarifa kwa viongozi anapohama au kusafiri kwa muda mrefu, anapobadili anuani, number ya simu, barua pepe na warithi.
- Kutoa taarifa za shida/msiba kwa kiongozi husika ili kuendelea na mchakato.
- Kuhakikisha ana kiasi cha $125 kwenye account ndani ya siku 30 ili kupatiwa pesa/rambirambi anayotakiwa kupatiwa katika kipindi cha siku 7 ya kutoa taarifa ya shida.
    - Akiba tangulizi (advance) kwa ajili ya kukaa kwenye akauti ya chama ($100).
    - Pesa ya uanachama kila mwaka ($25).
        - Kila mwanachama atatakiwa kutoa $25 kila mwezi wanne (April).

# IBARA YA SABA

## 7 MUUNDO WA CHAMA

Muundo wa uendeshaji wa chama utakuwa wa ngazi tatu za vikao/mikutano kama ufuatavyo:

### 7.1 Mkutano Mkuu

Kutakuwa na mkutano mkuu wa chama utakaofanyika mara moja kwa mwaka (March). Maamuzi yataafikiwa kwa wingi wa kura za wanachama.

7.1.1 Majukumu ya mkutano mkuu:

- Kuchagua viongozi wa chama ikiwa muda wa uchaguzi umefika.
- Kupokea taarifa ya utendaji wa chama na mipango ya mwaka unaofuata.
- Kupokea taarifa za mapato na matumizi kwa mwaka mzima.
- Kufanya marekebisho kwenye miongozo na vifungu mbali mbali vya katiba ikiwa muda wa marekebisho umefika.
    - Katiba hurekebishwa kila baada ya miaka 2.

### 7.2 Mkutano wa Kamati ya Utendaji

Kutakuwa na mikutano itakaofanyika mara moja kwa mwezi. Maamuzi yataafikiwa kwa wingi wa kura za viongozi wa kamati ambao ni lazima kura zisiwe chini ya asilimia 50 (50%).

7.2.1 Majukumu ya mkutano wa kamati ya utendaji

- Chombo kikuu cha kusimamia masuala yote ya kila siku ya chama.
- Kuandaa, kuratibu, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa mipango ya chama.

- Kuandaa na kufanya maboresho ya kanuni na taratibu mbalimbali zitakazotumika kuendesha chama na kuwasilisha kwa Bodi na wanachama.
- Kusimamia taratibu na kanuni za chama.
- Kuwasilisha taarifa za utendaji, utekelezaji na maendeleo ya chama kwenye mkutano mkuu wa chama.
- Kujadili maombi ya wanachama wapya.
- Kupokea, kujadili na kutoa mapendekezo ya mabadiliko ya katiba kama itakavyo jitokeza.
- Kujadili na kupendekeza agenda kwa ajili ya mkutano wa nwisho wa mwaka.

### 7.3 Mkutano wa Bodi

Kutakuwa na mikutano itakaofanyika mara nne kwa mwaka. Maamuzi yataafikiwa kwa wingi wa kura za wajumbe wa Bodi ambao ni lazima kura zisiwe chini ya asilimia 50 (50%).

7.3.1 Majukumu ya mkutano wa Bodi

- Kushauriana na kutatua matatizo yatakayojitokeza kwenye chama.
- Kupokea taarifa ya utendaji wa chama na mipango inayofuata.
- Kushughulikia masuala yanoyohusu wanachama/viongozi yanayojitokeza.
- Kujadili mapendekezo na hoja tofauti zinazohusiana na chama.
- Kubadilisha au kurekebisha vipengele vya katiba pale inapohitajika kwa kushauriana na wanachama.
- Kujadili na kupendekeza agenda kwa ajili ya mkutano wa mwisho wa mwaka.
- Kusitisha uanachama/uongozi kama utajitokeza.

**Uangalizi:** Mikutano ya dharura inaweza kufanyika kwa ngazi zote tatu pale ambapo itaonelea umuhimu wa kufanyika. Agenda, mahali/aina ya mkutano na muda vitatolewa mapema na Mwenyekiti.

## <u>IBARA YA NANE</u>

### 8 UTARATIBU WA KUENDESHA MIKUTANO

- Mikutano yote itatolewa taarifa ya kufanyika ndani ya siku kumi na nne (14) kabla ya kufanyika.
- Agenda pendekezwa zitawekwa wazi kwa wanachama wote ili wenye agenda za ziada waweze kuziwakilisha kwa Makamu wa Mwenyekiti kwa uchambuzi na mapitio siku tatu (3) kabla ya kikao.
- Vikao vya dharura kwa kamati zote vinaweza kuitishwa kulingana na mahitaji pasipo kigezo cha kutoa taarifa rasmi katika kipindi kilichowekwa.
- Muhutasari wa kikao utaandaliwa na kusomwa kwenye mkutano au kikao kikuu.

# IBARA YA TISA

**9 TARATIBU ZA KUPIGA KURA KATIKA UCHAGUZI**

- Kura zitapigwa kwa siri/wazi iwapo kutakuwa na mpinzani.
- Kila mwanachama hai mwenye akiba tangulizi (Advance) atakuwa na haki ya kupiga kura.
- Endapo ikatokea kura kulingana mara mbili mfululizo, Mwenyekiti ana haki ya kutumia kura ya turufu ili mshindi aweze kupatikana.
- Mgombea/Mada yeyote lazima apate/ipate kura nyingi zaidi ya wengine/nyingine ili kuweza kutangazwa kwa ushindi.

# IBARA YA KUMI

**10. UONGOZI WA CHAMA**

10.1 **MKURUGENZI MTENDAJI**

10.2 **KAMATI YA UTENDAJI**

- MWENYEKITI
- MAKAMU WA MWENYEKITI
- KATIBU/MHAKIKI
- MWEKA HAZINA
- AFISA UHUSIANO

10.3 **BODI YA WADHAMINI**

- MWENYEKITI
- KATIBU
- WAJUMBE (3)

10.4 **VIONGOZI WA KLUBS**

Kwa kuzingatia ibara ya 10, klub hizi zitafanya kazi na kuongozwa na viongozi kama ifuatavyo:

- BURUDANI (Entertainment)

  Klub hii hushughulika na maandalizi ya sherehe ya chama ambayo hufanyika kila mwaka (mwanzo/kati ya December). Sherehe hii ni kwa ajili ya wanachama wote pamoja na ndugu jamaa na marafiki wenye umri kuanzia miaka 22 kwenda juu. Klub hii itaongozwa na viongozi 3 na itakuwa ikisaidia klubs zingine au wanachama watakaohitaji msaada kwenye shughuli zao.

- BIMA (Insurance)

  Klub hii ni ya wanachama watakaopenda kujiunga na kufata sheria watakazojiwekea. Klub hii ni kwa ajili ya bima tofauti tofauti kama afya, maisha, vifo na magari.

- RAHA (Enjoyment)

Klub hii ni ya wanachama watakaopenda kujiunga na kufata sheria watakazojiwekea. Klub hii ni kwa ajili ya kufurahi kwa pamoja hasa kwenye birthdays, baby shower, harusi, bridal showers na kadharika.

- WATOTO (Kids)

Klub hii ni ya watoto wa umri kati ya mwaka mmoja (1) mpaka miaka kumi na mbili (12) ambao watakuwa wakikutana mara moja kwa mwaka hasa kipindi cha kiangazi (Summer). Klub hii ina malengo yafuatayo:

  - Kufahamiana.
  - Kucheza kwa pamoja.
  - Kujifunza mila na desturi za Kitanzania/Kimarekani.
  - Na kadharika.

- VIJANA (Teens)

Klub hii ni ya vijana wenye umri kati ya miaka 13 mpaka 21 ambao hukutana mara kwa mara kwenye mtandao wa ZOOM kwa lengo la kujifunza mambo mbalimbali ya kijamii. Vijana hawa watakuwa wakikutana mara moja kwa mwaka hasa kipindi cha kiangazi (Summer) kwa malengo ya:

  - Kufahamiana.
  - Kucheza kwa pamoja.
  - Kujifunza mila na desturi za Kitanzania/Kimarekani.
  - Na kadharika.

- WANAWAKE (Women's)

Klub hii ni ya wanawake watakaopenda kujiunga na kufata sheria watakazojiwekea. Klub hii ina malengo yafuatayo:

  - Kufahamiana.
  - Kubadilishana mawazo.
  - Kucheza kwa pamoja.
  - Kushirikiana katika shughuli na mipango mbali mbali ya maendeleo.
  - Na kadharika.

- WANAUME (Men's)

Klub hii ni ya wanaume watakaopenda kujiunga na kufata sheria watakazojiwekea. Klub hii ina malengo yafuatayo:

  - Kufahamiana.
  - Kubadilishana mawazo.
  - Kucheza kwa pamoja.
  - Kushirikiana katika shughuli na mipango mbali mbali ya maendeleo.
  - Na kadharika.

- UWEKEZAJI (Investment)

Klub hii ni ya mwanachama yeyote wa TSA atakaependa kujiunga na kuwekeza kwenye miradi mbali mbali. Wanachama hawa watakubaliana na kufata sheria watakazojiwekea. Makusanyo na mapato yanajadiliwa na wanachama wa Klub na si vinginevyo. Klub hii kwasasa inawekeza kwenye ukopeshaji kwa riba ndogo na inategemea kuja kuwekeza kwenye mambo mbali mbali yanayousiana na jamii kwa ujumla.

**Uangalizi:** Klub zote zitakuwa chini ya uangalizi wa viongozi wake na Mwenyekiti. Viongozi wa Klubs zote watawakilisha shughuli husika na zitategemea michango ya wanachama, ndugu, jamaa na marafiki. Iwapo kutahitajika msaada, chama kitajaribu kusaidia kitakapoweza.

## IBARA YA KUMI NA MOJA

### 11. SIFA NA MUDA WA UONGOZI

#### 11.1 Sifa za Kiongozi

- Anatakiwa kuwa mwanachama hai kwa muda usiopungua **miezi 6** na kwa mwanachama mwenye **ASILI au NASABA** ya utanzania kwa muda usiopungua **miezi 12**.
- Atakayeweza kusoma, kuzungumza na kuelewa kiswahili na kingereza.
- Anatakiwa kukubalika na viongozii/wanachama kwa wingi wa kura.
- Kutambua kuwa vikao vinaendeshwa kiswahili.
- Kuhakikisha ana $100 kwenye akaunti ya chama kama akiba.
- Kuwa mwaminifu, mvumilivu, jasiri, kujiamini, na kuwa na maono ya vitu mbalimbali.
- Kuwajibika kwa kutenda kazi na kujitolea.
- Kuongoza kwa kuonyesha mifano ya utendaji.
- Kukubaliana na wengi wape na kushirikiana sio vinginevyo.
- Kutokuwa na ubaguzi.
- Kutoonyesha hasira na kuamua kutoka kwenye uongozi/chama.
- Kujifunza na kukubali tofauti miongoni mwa watu na pia kukubali kurekebishwa iwapo utaonekana umekosea.
- Kuchangia topics zinazotakiwa kuchangiwa kimawazo.
- Kutotawanya habari/sauti (siri) zinazohusiana na uongozi nnje ya uongozi.
- Kukubali kuacha uongozi pale itakapoonekana umeshindwa kutekeleza matakwa ya watu wote.

### 11.2 Muda wa Uongozi

- Viongozi watachaguliwa wakati wa mkutano mkuu (March) na uongozi utadumu madarakani kwa muda wa miaka miwili (2) toka tarehe ya uchaguzi.
  - Mkurugenzi Mtendaji ataendelea na uongozi bila kubadilishwa.
  - Ikitokea kiongozi kutaka kujiudhuru kabla ya wakati au kupoteza maisha yake
    - Atatakiwa kutoa taarifa (kwa maandishi) wiki mbili kabla ya kujiudhuru.
    - Bodi ya Wadhamini inaweza kuteua kiongozi wa muda kukaimu nafasi hiyo mpaka uchaguzi ujao.
- Kiongozi yeyote anaruhusiwa kuendelea madarakani iwapo hakutakuwa na kiongozi wa kujitolea katika sehemu husika.

### 11.3 Sababu za kusimamishwa Uongozi

11.3.1 Kiongozi atasimamishwa iwapo atafanya yafuatayo:

- Kutoheshimu uongozi/wanachama.
- Kutumia lugha isiyo sahihi.
- Kufuja mali/pesa za chama.
- Kutokuwa na $100 kwenye akaunti ya chama kama akiba kwa muda wa siku zaidi ya 30.
- Kuleta mambo binafsi kwenye chama na kuanzisha malumbano yasiohusiana na uongozi.
- Kushabikia mambo binafsi na kuendeleza malumbano zaidi ya mara 3.
- Kutoonyesha mifano ya utendaji na kutawanya habari/sauti (siri) zinazohusiana na uongozi nnje ya uongozi.
- Kubadilisha mawazo tofauti na makubaliano ya viongozi (wengi wape).
- Kutochangia mada zinazotakiwa kuchangia zaidi ya mada 3.

11.3.2 Kiongozi atapewa warning zifuatazo:

- Kutaarifiwa kuwa amekosea na Makamu wa Mwenyekiti/Mwenyekiti.
- Kuandikiwa barua na Mwenyekiti.
- Kukutana na wajumbe wote wa Bodi.
  - Atatolewa kwenye uongozi kwa muda wa siku 90 (miezi 3) na kurudishwa
- Atasimamishwa uongozi akirudia makosa na kutoruhusiwa kuwa kiongozi tena.

# IBARA YA KUMI NA MBILI

## 12. WAJIBU WA VIONGOZI WA KAMATI YA UTENDAJI

Viongozi wote watafanya kazi mara baada ya kuchaguliwa. Wote kwa pamoja watawajibika kama ifuatavyo:

### 12.1 **MKURUGENZI MTENDAJI -** (CEO)

- Kusimamia na kuangalia mwenendo wa chama na bodi.
- Kufanya kazi kwa karibu na Wenyeviti (Kamati & Bodi).
- Kutatua matatizo yatakayojitokeza kati ya Kamati na Bodi.

### 12.2 **MWENYEKITI -** (President)

- Kuongoza na kuangalia mwenendo wa chama.
- Kuongoza vikao vikuu vya chama.
- Kushughulikia masuala yote ya chama.
- Kufanya kazi kwa karibu na viongozi wote.
- Kuidhinisha bajeti ya chama kwa kushirikiana na Bodi ya Wadhamini.
- Kutoa idhini ya mwisho ya matumizi ya chama
- Kufanya kazi kwa karibu na Mwenyekiti wa Bodi.
- Kutoa maamuzi wa mwisho iwapo kura zitagongana.
- Kushiriki kikamilifu kwa kutoa michango na mawazo katika vikao na shughuli zote za chama.

### 12.3 **MAKAMU WA MWENYEKITI -** (Vice President)

- Kuongoza vikao vya kamati ya utendaji.
- Kufanya kazi kwa karibu na viongozi wa kamati ya utendaji.
- Kuongoza vikao na kutoa ripoti za mikutano ya kamati ya utendaji.
- Kuweka kumbukumbu zote za vikao vya chama kwa usahihi.
- Kushiriki kikamilifu kwa kutoa michango na mawazo katika vikao na shughuli zote za chama.

### 12.4 **KATIBU/MHAKIKI** – (Secretary General/Reviewer)

- Kushughulikia na kuidhinisha shughuli yoyote inayohusu mwanachama.
- Kutoa taarifa zozote za mwanachama na matukio yote (shida/misiba).
- Kuwa na kumbukumbu za wanachama wote.
- Kufanya kazi kwa ukaribu na Mweka Hazina.
- Kushiriki kikamilifu kwa kutoa michango na mawazo katika vikao na shughuli zote za chama.

12.5 **MWEKA HAZINA** – (Treasurer)

- Kukusanya michango ya chama kama itakavyokuwa imekubalika na kuhitajika.
- Kuandaa bajeti ya chama na kuidhinisha matumizi ya chama.
- Kukagua na kuidhinisha matumizi ya chama
- Kutoa taarifa ya mapato kila mwezi na wakati wa kufunga shida/misiba.
- Kutoa pesa kwa wenye shida/misiba.
- Kutoa pesa kwa shughuli zinazohusu chama.
- Kutoa taarifa ya matumizi ya chama.
- Kuweka kumbukumbu sahihi za michango ya chama.
- Kuweka kumbukumbu na risiti za matumizi yanayohusu chama.
- Kuibua njia mpya za mapato ya chama.
- Kufanya kazi kwa karibu na Katibu/Muhakiki.
- Kufanya kazi kwa karibu na Mwenyekiti na watia saini.
- Kuhakikisha nakala za upokeaji wa pesa zimejazwa kikamilifu na kuwa na sahihi zote.
- Kufile Income Tax IRS Form 990.
- Kuwa mwaminifu na kutotumia pesa za chama.
- Kushiriki kikamilifu kwa kutoa michango na mawazo katika vikao na shughuli zote za chama.

12.6 **AFISA UHUSIANO – (**Public Relations Officer)

- Kukagua na kutangaza matangazo siku zisizokuwa za matangazo.
- Kutoa taarifa za chama kwenye mitandao ya kijamii.
- Kutangaza na kukaribisha wageni.
- Kutoa mafunzo kwa wageni.
- Kushiriki kikamilifu kwa kutoa michango na mawazo katika vikao na shughuli zote za chama.

## IBARA YA KUMI NA TATU

### 13. WAJIBU WA VIONGOZI WA BODI YA WADHAMINI

Viongozi wote watafanya kazi mara baada ya kuchaguliwa. Wote kwa pamoja watawajibika kama ifuatavyo:

13.1 **MWENYEKITI** (Chair of the Board)

- Kuongoza vikao vikuu vya Bodi.
- Kufanya kazi kwa karibu na Katibu/Wajumbe.
- Kushauriana na Katibu/Wajumbe na kutatua matatizo yatakayojitokeza kwenye chama.

- Kuandaa na kuhakikisha sheria zinapitishwa na wajumbe ili zitumike na chama.
- Kuangalia kwa umakini utendaji wa kazi kwa katibu na wajumbe wa Bodi.
- Kumsimamisha kiongozi wa Bodi, Kamati ya Utendaji/Mjumbe yeyote asiyefata sheria.
- Kushirikiana na Mwenyekiti/Mkurugenzi Mtendaji kwa kuhakikisha sheria na matatizo ya chama yanafanyiwa kazi.
- Kushiriki kikamilifu kwa kutoa michango na mawazo katika vikao na shughuli zote za chama.

13.2 **KATIBU** (Secretary)

- Kufanya kazi kwa karibu na Mwenyekiti wa Bodi.
- Kutoa taarifa za mikutano ya Bodi.
- Kuweka listi ya Wajumbe wa Bodi na kumbukumbu za vikao vyote vya Bodi.
- Kufanya kazi kwa karibu na Mwenyekiti/Wajumbe.
- Kuhakikisha nakala zote ziko sahihi/vizuri na tayari kwa kutumika pale zinapotakiwa.
- Kushiriki kikamilifu kwa kutoa michango na mawazo katika vikao na shughuli zote za chama.

13.3 **WAJUMBE**

- Kufanya kazi kwa karibu na Mwenyekiti/Katibu.
- Kuidhinisha bajeti ya chama.
- Kushiriki kikamilifu kwa kutoa michango na mawazo katika vikao na shughuli zote za chama.

## IBARA YA KUMI NA NNE

**14. WAJIBU WA VIONGOZI WA KLUBS**

- Kuongoza na kuangalia mwenendo wa Klub.
- Kuleta maoni ya nini kifanyike kwenye Klub.
- Kushirikiana na Mwenyekiti kwa kuamua kwa pamoja nini kifanyike kwenye klub.

## IBARA YA KUMI NA TANO

### 15. VYANZO VYA MAPATO YA CHAMA

15.1 Vyanzo vya mapato ya chama hiki vitakua kama ifuatavyo:

- Ada ya uanachama ya kila mwanzo wa mwaka (April & Non refundable).
- Viingilio vya wanachama wapya kila mwezi (Non refundable).
- Harambee mbalimbali za kutunisha mfuko wa chama.
- Misaada kutoka kwa kampuni, watu binafsi, mashirika ya kitaifa na kimataifa yaliyo ndani na nje ya nchi.

15.2 Kwa kuzingatia ibara 15.1, wanachama wanauwezo wa kutoa njia mbadala ambazo zinaweza kutunisha mfuko wa chama, ila njia ziwe halali.

15.3 Pale itakapolazimu kufanyika ukaguzi wa mahesabu. Ukaguzi huu utafanywa na wakaguzi wenye sifa kulingana na sheria za Texas.

## IBARA YA KUMI NA SITA

### 16. FEDHA NA UENDESHAJI WA AKAUNTI ZA BENKI.

16.1 Kulingana na mwenendo wa chama, mapato yote yatakayopatikana katika chama yatahifadhiwa kwenye akaunti ya chama ambayo itakuwa chini ya Mweka Hazina, Mkurugenzi Mtendaji na Watia Saini wawili. Watia saini hao watakua na dhamana ya kutunza fedha hizo na kuhakikisha usalama wake.

16.2 Michango yote ya chama itawekwa kwenye akaunti ya chama na wanachama husika na kumkabidhi receipt/ujumbe Muweka Hazina. Mwanachama anatakiwa kutuma michango yote kupitia

Jina la Benki: Wells Fargo
Jina la Akaunt: Tanzania Sharing Association
Benki Akaunti Namba: 7975995742

**Zelle Information**
Jina: Tanzania Sharing or Tanzania Association
Telephone: 281-372-9205
Benki Akaunti Namba: 7975995742

**Cashapp Information**
Cashapp: $TSAssociation
Telephone: 281-372-9205

16.3 Wanachama watapokea taarifa za mapato ya shida/msiba mara moja kwa mwezi (Kati ya tarehe 1-5) na wakati wa kufunga shida/misiba.

16.4 Mwanachama atapokea michango kwa kutumia njia tofauti tofauti zikiwemo Zelle/CashApp/Wire Transfer/Checks/Cashier's Checks/Money Order/ /Western Union/Wave/World Remit.

16.5 Fedha zote zitatumika katika shughuli za kijamii zikiwemo shida/misiba itakayotangazwa na Muhakiki.

## IBARA YA KUMI NA SABA

**17. MICHANGO**

17.1 Ada ya uanachama $25 kila mwanzo wa mwaka (April & Non refundable)

17.2 Mwanachama atachangia shida/misiba pale taarifa ya mwanachama/ndugu itakayokubaliwa na KAtibu/Muhakiki na kutangazwa kwenye chama **(3,000/jumla ya wanachama hai)** ndani ya majuma mawili.

- Mwanachama atachangia misiba/shida 3 mpaka 5 ndani ya mwezi na sio zaidi ya $100.
    - Ikiwa zaidi ya misiba/shida 5 au $100, mwanachama atachangia misiba mingine mwezi unaofata.

17.3 Mwanachama atachangia pale taarifa ya kifo cha Mwanachama/Mtoto itakapotangazwa kwenye chama **(10,000/jumla ya Wanachama hai)** ndani ya majuma mawili.

- Mtoto wa chini ya miaka 21 aishio jimbo lolote ndani ya USA.
- Mwanachama atachangia misiba 2 mpaka 3 ndani ya mwezi na sio zaidi ya $200
    - Ikiwa zaidi ya misiba 3 au $200, mwanachama atachangia misiba mingine mwezi unaofata.

17.4 Mwanachama atachangia raha zilizowekwa kwenye **SHERIA** kwa **HIARI**.

17.5 Mwanachama asipochangia **shida/msiba 3** bila taarifa yeyote/isiojitosheleza, atakuwa amevunja sheria ya chama na hivyo amejitoa katika chama bila kurudishiwa pesa ya nyuma aliyokwisha changia.

- Shida/msiba wa kwanza atapewa **ONYO**, shida/msiba ya pili atatoa **$15** kama adhabu ya kuchelewa na shida/msiba wa 3 atatolewa.
    - Adhabu hizi zitaisha ndani ya mwaka na kuhesabika upya iwapo mwanachama atarudisha michango yote aliokosa kuchangia.
    - Mwanachama hataruhusiwa kurudi ndani ya mwaka mmoja na pindi atakapotaka kurudi atatakiwa kurudi kama mwanachama mpya.
- Mwanachama aliechangiwa, atatakiwa kurudisha pesa aliyochangiwa (Pesa aliochangiwa – Pesa aliochanga).

- Iwapo mwanachama atakataa kurudisha pesa au kugundulika ametoa habari za uongo
    - Mwanachama atachukuliwa hatua kisheria na kutangazwa kwenye vikundi vingine kama fundisho.
    - Mwanachama hataweza kusaidiwa tena katika shida/raha zake na mwanachama wa TSA.
        - Mwanachama wa TSA akionekana kumsaidia kwa namna moja au nyingine, nayeye atatolewa kwenye chama na kurudishiwa akiba tangulizi (advance).

**Uangalizi:** Michango itabadilishiwa iwapo kutahitajika na uongozi/wanachama.

## IBARA YA KUMI NA NANE

**18. MAFAO KWA MWANACHAMA**

18.1 Kufariki kwa mwanachama/mtoto wa umri chini ya 21 – **USD 10,000/$5,000/$2,000.**

18.2 Kupata shida/msiba kwa ajili ya mwanachama na ndugu – **USD 3,000/$1,500/$500.**

18.3 Ukizingatia Ibara ya 18.1 & 18.2, mwanachama atapokea mafao yake

- Baada ya Mweka Hazina kuhakikisha kama mwanachama ana **$125** kwenye akaunti ya chama
    - Ikiwa chini ya $125 (Akiba tangulizi & ada ya uanachama), mwanachama atakabidhiwa **$1,500** na familia itasaidiwa **$5,000**.
    - Ikiwa ana **$0** kwenye akiba tangulizi (advance) ila ana **$25** ada ya uanachama, mwanacha atakabidhiwa **$500** na familia itasaidiwa **$2,000.**
    - Ikiwa hana pesa kwenye account, mwanachama/familia watachangiwa kihiari.
- Baada ya Katibu/Mhakiki kuridhia na kutangaza shida/msiba.
- Baada ya kutoa taarifa za matumizi/upokeaji wa pesa na kutia saini mkataba wa kupokea pesa.
    - Warithi watakuwa na mkutano na viongozi wa TSA kwa kushauriana jinsi ya kusaidiwa/kukabidhiwa rambi rambi.
- Jumla ya shida ni 5 ndani ya miaka 5 (2025)
    - 2 shida ikiwemo msiba ndani ya mwaka.

## IBARA YA KUMI NA TISA

**19. SHERIA NDOGONDOGO NA UREKEBISHAJI WA KATIBA**

19.1 Uongozi wa chama utatakiwa kutengeneza sheria ndogondogo za chama ili kuwezesha chama hiki kuendelea vizuri.

19.2 Sheria ndogondogo zote zitaanza kutumika mara baada ya kutungwa na kukubalika na wanachama kwa kuanza kutumika.

19.3 Ibara zinazounda katiba hii na sheria ndogondogo za chama zinaweza kufutwa na/au kurekebishwa baada ya nusu ya wajumbe wa chama kupitisha pendekezo hilo.

19.4 Sheria zozote zilizotumika miaka ya nyuma, haziruhusiwi kurudishwa katika katiba.

19.5 Katiba hii inaweza kufanyiwa mabadiliko kila baada ya miaka 2 kwa kuongeza vifungu au kuboresha vilivyopo. Mabadiliko au marekebisho ya katiba yanaweza kufanywa kwa azimio la wanachama litakaloungwa mkono na 2/3 ya wanachama katika mkutano mkuu.

## IBARA YA ISHIRINI

**20. KUVUNJIKA KWA CHAMA;**

Iwapo litajitokeza jambo lolote litakalopelekea chama hiki kuvunjika au kuvunjwa, azimio hilo la kuivunja chama lazima liwe limeungwa mkono 2/3 ya wanachama hai wa mkutano mkuu. Mara baada ya azimio hilo kupitishwa, utafanyika utaratibu wa kutathmini mali zilizopo. Iwapo kutakuwa na madeni, madeni hayo yatalipwa kwanza na mali zitakazobakia zitagawanywa kwa wanachama hai kwa usawa.

## MWISHO

**MAKUBALIANO YA KATIBA**

***Katiba hii imerekebishwa na mkutano mkuu March/June 2021 na kuanza rasmi April/July 2021.***

Mimi …………………….……………………………………. mwanachama wa

Tanzania Sharing Association, ninakubali kuisoma, kuielewa na kukubaliana na sheria

zilizowekwa kwenye Katiba hii.

……………………………………. ………………………………..

Saini Tarehe

………………………. ……… … …………………………….. ……………………..

Mwenyekiti & Mkurugenzi Mtendaji Saini Tarehe

………………………. ……… … …………………………….. ……………………..

Makamu wa Mwenyekiti Saini Tarehe

………………………. ……… … …………………………….. ……………………..

Katibu/Mhakiki Saini Tarehe